# Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Mshikamano wa Kitaifa

*Mutahi Miricho*[1], *Sheila P. Wandera-Simwa*[2] na *Nabea Wendo*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Chuka, Kenya*
[2]*Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya*

**Ikisiri**

**Makala haya yanabainisha nafasi ya Fasihi ya Watoto katika mshikamano wa kitaifa. Waandishi wamerejelea vitabu teule vya fasihi ya watoto ambavyo ni *Urembo wa Ngiri* (2016) na *Sungura Mpanda Ngazi* (2008). Mshikamano wa kitaifa nchini Kenya umekuwa ukitikiswa hasa kutoka mwaka wa 2007/2008 wakati ghasia zilizuka baada ya Uchaguzi Mkuu. Tangu wakati huo wameibuka waandishi wapya wanaoandikia masual ya fasihi ya watoto ambayo licha ya kuburudisha ina dhima na mielekeo mipya inayolenga kukuza utaifa na mshikamano. Makala haya yanalenga kuthibitisha kuwa fasihi ya watoto imechukua mielekeo mipya ambapo, sawia na fasihi ya watu wazima, inatekeleza dhima muhimu katika uhamasisho wa kisiasa na mshikamano wa kijamii.**

**Maneno Muhimu:** Fasihi ya Watoto, Utaifa, Mshikamano.

## Utangulizi

Makala haya yanaangazia dhima ya fasihi ya watoto ya Kiswahili katika mshikamano wa kitaifa. Fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto (Ngugi, 2012). Kwa muda mrefu, fasihi ya watoto imeelekea kuepuka masuala yanayohusu itikadi za kisiasa labda ikichukuliwa kama yanayofaa kushughulikiwa tu katika fasihi ya watu wazima. Wataalamu kama vile Bhroin na Kennon (2012) wamejishughulisha na udadisi kuhusu masuala yanayofaa pamoja na yasiyofaa kuandikiwa watoto. Kati ya masuala mengine, wanachunguza ni mambo gani wanayoelezwa watoto kuhusiana na uraia na itikadi. Kwa upande mwingine, Hunt (1988) anadai kuwa fasihi ya watoto inapaswa kudhibitiwa, kwa njia hii, tunaweza kuchuja mambo ambayo watoto huambiwa kupitia fasihi hii.

Aidha, makala haya yamechochewa na maoni ya wataalamu kama vile Puurtinen (1998) na Ngugi (2016). Puurtinen amedai kuwa fasihi ya watoto ina umuhimu mkubwa katika kuelekeza itikadi za watoto lakini imepuuzwa katika tafiti za kiusomi. Ngugi (2016) anaelekea kuchochea wazo hili kwa kuhimiza upanuzi wa masuala ambayo fasihi ya watoto inashughulikia kimaudhui na

kupendekeza ijumuishe masuala ibuka na halisi yanayojitokeza katika jamii kiwakati. Mtaalamu huyu wa fasihi ya watoto anaeleza kuwa fasihi ni zao la wakati, na jinsi jamii inavyobadilika ndivyo fasihi inavyobadika ili iweze kuyamulika masuala mapya yanayoibuka katika jamii. Maoni haya yameupa msukumo utafiti uliotangulia makala haya kushughulikia masuala ibuka yanayotokana na itikadi za kisiasa zinazoathiri uchaguzi mkuu nchini Kenya.

Tangu 2007 wakati ghasia zilizuka nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu, umoja na mshikamano wa kitaifa umekuwa ukitikiswa kutokana na matamshi ya chuki yanayosababisha mgawanyiko. Hollindale (1988) anaeleza kuwa dhana ya itikadi katika fasihi ya watoto inajitokeza kutokana na mwelekeo wa mwandishi. Mambo anayoamini mwandishi kuhusu siasa, jamii na maadili hujitokeza katika hadithi anayowaandikia watoto na huwa kama anawapendekezea watoto mawazo yake kupitia hadithi husika. Nguvu za itikadi zinazohisika katika hadithi huaminika kuwa zinazunguka katika akili ya msomaji anaposoma na zinaweza kuathiri mtazamo wake. Kwa mantiki hii, itikadi za kisiasa zikipitishwa kupitia hadithi za watoto zinaweza kumwaathiri motto ambaye ataweza kuchukua mielekeo fulani ya kisiasa kutokana na hadithi alizosoma.

**Muhtasari wa Hadithi Zilizoteuliwa**

Vitabu vya fasihi ya watoto vilivyoteuliwa kwa uhakiki ni vile ambavyo vinaonekana kupata msukumo wake kutokana na siasa za nchi ya Kenya. Vitabu hivyo ni pamoja na: *Urembo wa Ngiri* (2016) na *Sungura Mpanda Ngazi* (2008). Hadithi katika vitabu hivi zinaelekea kuleta upya fulani katika fasihi ya watoto na kudhihirisha kuwa katika miaka ya hivi karibuni, uandishi wa fasihi ya watoto umebadilika na fasihi hii imechukua mielekeo mipya. Itikadi za kisiasa na mamlaka zinaanza kujipenyeza katika hadithi za watoto hasa kuhusiasa na siasa za uchaguzi mkuu nchini Kenya. Watoto wanaolengwa katika vitabu hivi ni wale wa kati ya miaka tisa na kumi na miwili.

**Muhtasari wa *Urembo wa Ngiri***

*Urembo wa Ngiri* (2016) ni hadithi inayohusu mgogoro unaowakumba wanyama nyikani kutokana na mashindano ya urembo. Mashindano hayo yalishindwa kuwatambulishia mshindi, kwani walikosa kukubaliana. Kulingana na matokeo yaliyotangazwa, chui ndiye alishika mkia. Aliyapinga matokeo hayo na kudai kuwa alinyang'anywa ushindi. Akadai kuwa kura zake zimeibiwa. Chui alikataa kutambua ushindi wa Ngiri. Vita vilizuka baina ya wafuasi wa Chui na wafuasi wa Ngiri. Chui alichochea wafuasi wake kuchoma makazi ya Ngiri ili kumfukuza nyikani. Wanyama wenye madoadoa waliwafukuza wale wasio na madoadoa nyikani. Ilimbidi Ngiri ahamie msituni pamoja na wanawe na kuishi kama mkimbizi. Mwishoni mwa hadithi hii safari ya maridhiano inaanza.

### Muhtasari wa *Sungura Mpanda Ngazi*

*Sungura Mpanda Ngazi* (2008) ni hadithi inayotokana na mgogoro kati ya Sungura na wanyama wenzake. Sungura alikuwa amesaidiwa na wanyama kuukwea mwembe kwa ahadi kuwa akifika juu ya mwembe angewaangushia wanyama wenzake maembe. Alipoyafikia, aliyala peke yake bila kuwaangushia wanyama hata embe moja.

### Maudhui ya Kisiasa

Siasa ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Maamuzi ya kisiasa yanayofanywa huelekeza sera za maendeleo ya nchi na hivyo ustawi wa nchi hutegemea maongozi ya kisiasa yaliyomo. Katika jamii nyingi, siasa ni za watu wazima na hivyo huepukwa katika fasihi ya watoto. Hata hivyo, katika hadithi ya *Urembo wa Ngiri* (2016) na *Sungura Mpanda Ngazi* (2008), mtunzi amekiuka matarajio na kuzingatia siasa katika hadithi zake za watoto. Ukiushi huu umeleta mwamko mpya katika fasihi ya watoto. Tutatathmini maudhui ya kisiasa tunayochanganua kupitia mtazamo wa nadharia ya uhalisia tukiegemea mhimili wake mkuu ambao ni matukio yenye kuakisi maisha halisi ya jamii. Mhimili huu utayafaa makala haya katika kutathmini uhalisia wa maudhui ya kisiasa unavyobainika katika fasihi ya watoto kwa kuchunguza masuala ya maudhui na uhusiano wake na matukio halisi ya kisiasa katika jamii ya mwandishi ambayo ni jamii ya Kikenya.

### Masuala ya Kisiasa yanayochochea Maudhui katika Hadithi za Watoto

Masuala mbalimbali ya kisiasa yanaendelezwa katika hadithi ya *Urembo wa Ngiri* (2016) na *Sungura Mpanda Ngazi* (2008). Kwa kutumia mtazamo wa nadharia ya uhalisia tukiegemea mhimili wake mkuu ambao ni matukio yenye kuakisi maisha halisi ya jamii, tunapata kwamba masuala hayo ya kisiasa yanahusiana na hali halisi katika jamii ya nchi ya Kenya. Masuala ya kisiasa yanayochochea maudhui katika hadithi za watoto katika vitabu hivi viwili yana uhusiano mkubwa na Uchaguzi Mkuu nchini Kenya ambako ndiko mwandishi wa hadithi anaishi. Masuala haya yanaweza kuchunguzwa katika vitengo viwili. Kuna masuala yanayohusu matukio ambayo yanashuhudiwa kabla ya uchaguzi na yale yanayohusu matukio ya baada ya uchaguzi.

### Kabla ya Upigaji Kura

Kabla ya upigaji kura huwepo na kipindi cha kampeni. Kipindi hiki hushuhudia utoaji wa ahadi nyingi na wale wanaowania viti, unafiki na uongo pamoja na tamaa na ubinafsi.

### Kampeni

Katika S*ungura Mpanda Ngazi*, wanyama wanapohitaji kuyala matunda wanaulizana namna ya kuyafikia. Fisi alishauri kuwa watafute mawe walenge yale maembe mabivu na yakianguka wa kwanza kula awe ni yeye Fisi. Hapo Fisi

akawa anajipigia debe. Baadaye, Sungura aliwaambia wanyama kuwa alikuwa na wazo kuwa watengeneze ngazi kisha wamshikie mmoja wao ili apande na akiwa juu awaangushie matunda yaliyoiva. Wanyama walipokubali wazo hili, mara moja Sungura alisema angekwea. Hapo Sungura naye akawa anajipendekeza achaguliwe na wanyama wenzake. Ingawa wanyama wengine walinung'unika, Sungura aliendelea na kampeni za kutaka achaguliwe kuyafikia matunda kwa kudai kuwa alikuwa amejitolea kuwasaidia. Sungura akawaomba wamsaidie kukwea huku akitoa ahadi kuwa akifika juu hangewasahau na kwamba angewaangushia maembe. Katika kampeni zake, alitoa mwito wa umoja akionyesha kuwa kwa umoja wao wataweza kupata matunda. Anasema:

> Kama mjuavyo, siwezi kuukwea mwembe huu kwa uwezo wangu. Ninahitaji usaidizi wenu, umoja wetu ni nguvu zetu. Kwa umoja wetu, tutaweza kuyapata maembe. Nyinyi mnishikie ngazi, nami niipande (uk. 9).

Wanyama waliamini maneno matamu ya Sungura na wakakubali kumtengenezea ngazi ambayo ingemwezesha kupanda mwembe.

### Unafiki na Uongo

Kabla ya Uchaguzi Mkuu wawania nyadhifa za uongozi huwatolea wapiga kura ahadi nyingi katika juhudi za kujipendekeza kwa wananchi na kuonyesha jinsi walivyo na uwezo wa kuwasaidia. Viongozi kama hao hutumia matatizo yanayokabili jamii kama fursa yao ya kuonyesha jinsi watakavyoyatatua wakichaguliwa kama vile Sungura alivyoahidi wenzake kuwa angewaondolea tatizo la njaa. Sungura alijitetea kwa unyenyekevu na upole achaguliwe yeye kupanda juu ya mwembe ili awaangushie wenzake maembe lakini alipofika juu akawasahau wanyama wenzake. Ahadi zake ziliishia kuwa ahadi za uongo na hakufanya lolote la kuwafaidi wenzake alipokuwa katika mamlaka juu ya mwembe.

Sawa na Sungura, kuna watu hasa wanasiasa wanaofanya kampeni wachaguliwe kupata mamlaka kama vile vyeo vyenye uwezo kama vile Ubunge, Useneta, Ugavana na Urais. Viongozi hao hutoa ahadi kuhusu maendeleo ambayo wangewaletea wananchi wenzao wangewasaidia kupanda ngazi ya mamlaka ya kisiasa lakini mara wanapopata maslahi yao wanawasahau wenzao waliowaweka katika nafasi hiyo wakiwa na matumaini kuwa watawasaidia.

### Tamaa na Ubinafsi

Tamaa na ubinafsi aghalabu hutokea kuwa viongozi wengi wanaowania viti mbalimbali. Hali hizi huwa ndani ya nafsi zao kiasi cha kuongozwa na tamaa na ubinafsi kwa kuwa huwa wanataka wao tu wachaguliwe. Ilivyo ni kuwa hawako tayari kuachia wenzao fursa ya kuchaguliwa. Mara nyingi, kuomba kura huwa ni njia ya kuwatumia wengine kujifaidi wao wenyewe kisiasa na kiuchumi. Hujifanya wanajitolea kwa maslahi ya wengine ilhali wajitolea kwa ajili yao

wenyewe. Katika *Sungura Mpanda Ngazi*, mnyama wa kwanza kujitolea kutoa pendekezo la suluhisho alikuwa Fisi. Fisi alishauri kuwa watafute mawe walenge yale maembe mabivu na yakianguka wa kwanza kula awe ni yeye Fisi. Wazo hili linadhihirisha kuwa Fisi aliongozwa na tamaa na ubinafsi. Katika jamii, viongozi wenye ubinafsi hutoa mapendekezo yatakayowanufaisha wao kwanza. Kadhalika, Fisi aliposhindwa kuyyangusha matunda, Sungura alipendekeza mnyama mmoja asaidiwe kuukwea mwembe. Wazo hili lilizua mjadala kuhusu uteuzi wa yule ambaye angeukwea mwembe. Hapo ndipo Sungura alijipendekeza. Wanyama wengine walinung'unika lakini Sungura akakazania kuwa ni yeye aliyekuwa tayari kuwasaidia. Sungura alisisitiza kuwa ndiye alifaa licha ya wanyama wenzake kulalamika. Bila shaka, aliongozwa na tamaa na ubinafsi. Hivyo, Fisi na Sungura wanaongozwa na ubinafi katika kujitolea kwao kusaidia kupata maembe. Katika siasa nchini Kenya, viongozi wa kisiasa, aghalabu, hukabiliana na wapinzani wao vikali kila mmoja alijipendekeza kwa raia na kutaka iwe ni yeye pekee atakayechaguliwa kuchukua mamlaka ya uongozi.

**Baada ya Upigaji Kura**

Baada ya upigaji kura, vitisho hutokana na wawania uchaguzi walioshindwa kukataa matokeo na badala yake, hutoa matamshi ya chuki, uchochezi. Kisha, makundi ya vijana wanaotumiwa kuzusha vurugu inayopelekea uharibifu wa mali na watu kujeruhiwa na hata kuuawa. Hatimaye, hujitokeza makundi ya watu wenye jukumu na juhudi za kutafuta maridhiano na amani.

**Walioshindwa Kukataa Matokeo**

Baada ya mashindano ya urembo kutangazwa katika *Urembo wa Ngiri,* wanyama wanakosa kukubaliana kuhusu matokeo, hali ambayo inazua mzozo. Ngiri aliibuka mshindi kwa kura 51. Wanyama walishangilia ushindi wake kwa vifijo na hoihoi lakini Chui aliposikia matokeo hayo ya kura, alizirai. Ngiri alikubali ushindi. Kulingana na matokeo yaliyotangazwa, chui ndiye alishika mkia. Hakuamini. Alipinga matokeo hayo na kudai kuwa alinyang'anywa ushindi. Akadai kuwa kura zake zimeibwa. Chui alikataa kuutambua ushindi wa Ngiri. Aliungwa mkono na Duma aliyedai kuwa kura zimeibwa ingawa hangeweza kuthibitisha madai yake. Chuki ilizuka baina ya Ngiri na Chui kutokana na madai haya.

Usiku wa manane, wanyama walipokuwa wanaendelea kusherehekea ushindi wa Ngiri, Chui akiamdamana na wanyama waliomuunga mkono kama vile Duma, alifika ukumbini kutoka msituni. Akajitoma ukumbini na kuzusha sokomoko. Duma na Chui walitamka matamshi yaliyowaudhi wanyama waliokuwa wanasherehekea ushindi. Walisema ushindi wake ulitokana na wizi na hivyo, walihapa kuwa hawangeukubali. Chui alisema kuwa hakutakuwa na amani kama hatakabidhiwa ushindi.

Matamshi haya ya chuki yalichemsha akili za baadhi ya wanyama na kuzusha rabsha. Viti vilivyokuwa ukumbini viligeuzwa kuwa zana za vita na kurushwa kote ukumbini na kusababisha mapigano makuu. Chui alimchapa kofi Ngiri naye ngiri akalipiza kisasi kwa kumpiga Chui kwa kichwa. Ghasia ikawa imezuka ukumbini licha ya Fisi kujaribu kuwa mpatanishi na Nyati, aliyesimamia uchaguzi, kusisitiza kuwa Ngiri alikuwa ameshinda kihalali na hakukuwa na udanganyifu wowote. Wanyama wakaumizana wenyewe kwa wenyewe. Ilikuwa ni vita za wafuasi wa Chui dhidi ya wafuasi wa Ngiri.Baadaye vita hivi vilitoka ukumbini na kufika hadi nyikani katika makao ya wanyama. Chui alichochea wafuasi wake kuchoma makazi ya Ngiri ili kumfukuza nyikani. Walipanga kumchoma Ngiri na wanawe wakiwa wamelala ili kuangamiza kizazi cha Ngiri. Mipango yake iligunduliwa na Ngiri na ikaambulia patupu. Hata hivyo, Chui na wafuasi wake walianza maandamano waliyodai kuwa ni ya amani lakini ni maandamano ambayo yalisababisha kifo cha baadhi ya wanyama kama Fungo na Nyumbu pamoja na kung'olewa kwa nyasi iliyokuwa chakula cha Ngiri. Wanyama walikosa chakula na kukabiliwa na njaa.

Vita dhidi ya Chui na Ngiri vikachukua mwelekeo mpya na kuwa vita vya wanyama wenye mafumba dhidi ya wenye kwato. Vikawa pia vita baina ya wanyama wenye madoadoa na wale wasio na madoadoa. Wanyama ambao walikuwa wameishi kwa amani waligeukana na kupigana vita vikali na kuuana bila sababu. Amani haikuwepo tena. Wanyama wenye madoadoa waliwafukuza wale wasio na madoadoa nyikani na kuwafukuza hadi msituni. Nyikani kulikuwa hakukaliki na ilimbidi Ngiri ahamie msituni pamoja na wanawe na kuishi kama mkimbizi. Kwa mtazamao wa nadharia ya uhalisia hali hii inaweza kulinganishwa na hali halisi katika jamii ambapo katika mataifa mengi ya Kiafrika kumekuwepo na visa vya viongozi walioshindwa na wenzao katika uchaguzi mkuu kukosa kukubali kushindwa na badala yake kuzusha ghasia wakiteta bila ithibati ya kutosha kuwa kura zao zimeibwa.

Maudhui ya *Urembo wa Ngiri*, bila shaka yameathiriwa na hali sawa na hii ambayo ilitokea nchini Kenya baada ya uchaguzi wa 2007. Kulingana na ripoti ya Kriegler na Waki 2009, kufuatia kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Urais tarehe 30 Disemba 2007 ghasia zilizuka katika maeneo mbalimbali nchini Kenya kukiwa na madai kuwa iliyokuwa wakati huo Tume ya Uchaguzi ya Kenya-ECK ilikuwa imetumia udanganyifu katika uchaguzi wa Urais. Sawa na ripoti ya Kriegler na Waki, ripoti ya FIDA-K (2008) ilieleza kuwa Kenya ilifanya Uchaguzi Mkuu Disemba 27, 2007 ambao matokeo yake yaliyotangazwa tarehe 30 mwezi huo yalizua ghasia za ghafla wakati viongozi wa upinzani walioshindwa walipokataa matokeo yaliyotangazwa.

**Matamshi ya Chuki na Uchochezi**

Katika *Urembo wa Ngiri* Matamshi ya uchochezi ya Chui yalisababisha vurugu. Mzozo ulizuka wakati Chui alidai kuwa kura zake zimeibwa na kuwa Ngiri hakushinda kwa njia halali. Hali hii inaweza kulinganishwa na chuki za kikabila na matamshi ya chuki sawa na iliyoshuhudiwa wakati mtafaruku uliotokea nchini Kenya. Kriegler na Waki (2009) katika ripoti yao wanaeleza kuwa matamshi ya kikabila yaliyotolewa na baadhi ya wanasiasa yalichochea uhasama wa kabila moja dhidi ya jingine. Wanaendelea kusema kuwa ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka 2007 nchini Kenya zilichukua mwelekeo wa kikabila. Wanatoa mfano kuwa katika maeneo ya Bonde la Ufa na Pwani, vita vililenga jamii ya Wakikuyu na Wakisii kwa kuhusishwa na chama cha PNU kilichokuwa kimeonekana kunufaika na uchaguzi wa Urais ambao ulidaiwa ulikuwa na udanganyifu. Jamii nyingine ziliona kama zimenyang'anywa ushindi wa Urais huku pia zikidai kiongozi kutoka jamii yao ndiye alikuwa ameshinda. Kadhalika, FIDA –K (2008) inaeleza kuwa mkataba wa serikali ya mseto uliotiwa saini mnamo Februari 28, 2008 ulitambua kuwa vurugu zilizotokea kutokana na utata wa uchaguzi mkuu zilileta mgawanyiko mkubwa katika jamii ya Wakenya.

**Vita vya Kikabila**

Vita vya kikabila vimejadiliwa kwa mapana na marefu katika *Urembo wa Ngiri*. Kufuatia matamshi ya uchochezi ya Chui, vita dhidi ya Chui na Ngiri vikachukua mwelekeo mpya na kuwa vita vya wanyama wenye mafumba dhidi ya wenye kwato. Vikawa pia vita baina ya wanyama wenye madoadoa na wale wasio nayo. Wanyama ambao walikuwa wameishi kwa amani waligeukana na kupigana vita vikali na kuuana. Amani haikuwepo tena. Wanyama wenye madoadoa waliwafukuza wale wasio na madoadoa nyikani na kuwafukuza hadi msituni. Nyikani kulikuwa hakukaliki na ilimbidi Ngiri ahamie msituni pamoja na wanawe na kuishi kama mkimbizi.

Matukio katika hadithi hii yanaweza kulinganishwa na vita vya kikabila vilivyopelekea kufukuzwa kwa baadhi ya jamii kutoka maeneo fulani na kusababisha kuwepo kwa wakimbizi wa kisiasa wa ndani kwa ndani nchini Kenya baada ya kutokubaliana kuhusu mshindi na mshinde katika Uchaguzi Mkuu wa 2007. Kriegler na Waki, 2009 wanaeleza kuwa kati ya mambo yaliyosababisha mgogoro wa kisiasa nchini ni chuki za kikabila. Wanasema kuwa kutokana na madaraka makubwa yaliyokuwa katika Urais, kila jamii ilihisi kuwa inapaswa kupata nafasi ya mmoja wao kuwa Rais ili ijifaidi. Kriegler na Waki (2009) wanaeleza kuwa kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi, zaidi ya watu elfu mia tatu hamsini walifurushwa makwao na kuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani nchini. Kutokana na vurumai iliyotokea, zaidi ya watu elfu moja waliuawa na wengine wengi kupoteza mali yao. Haki za binadamu zilikiukwa kwa kiwango kikubwa katika ghasia hizo. Kulingana na ripoti hizi, ghasi hizi ziliendelea kwa

muda wa wiki nyingi na kusababisha vifo na uharibifu wa mali. Sawa na wanyama katika *Urembo wa Ngiri,* jamii mbalimbali za Wakenya zilizokuwa zimeishi kwa amani, umoja na upendo kabla ya Uchaguzi Mkuu zilivurugana mara tu baada ya uchaguzi.

**Usaliti**

Usaliti wa viongozi waliochaguliwa nchini unadhihirika katika *Sungura Mpanda Ngazi*. Usaliti unajitokeza Sungura anapobadilika na kuwageuka wanyama waliomsaidia kufikia matunda. Sungura alikuwa amewaahidi wanyama kuwa angewaangushia matunda akifika juu lakini badala yake alikula maembe yote bila kuwajali wanyama wenzake waliomkondolea macho na waliomtegemea awaondolee shida yao ya njaa. Hali hii ya Sungura kuonyesha usaliti kwa wanyama wenzake inaakisi matumizi mabaya ya mamlaka na ufujaji wa mali ya umma unaoendelezwa nchini na baadhi ya viongozi wa kisiasa waliochaguliwa. Viongozi wafisadi kama hao hutumia mali ya umma kama mali yao binafsi huku wananchi wakibaki katika umasikini. Kabla ya kufikia matunda, Sungura alikuwa mnyenyekevu lakini alibadilika alipofikia matunda akawa na kiburi, akawapuuza na kuwadharau wanyama wengine. Baadhi ya wanasiasa hubadilika na kuwapuuza wananchi waliowapigia kura wanaposaidiwa kupanda ngazi ya maisha kwa kuchaguliwa kuwa viongozi kama vile maseneta, wabunge au magavana. Hukosa kutimiza ahadi walizowatolea wananchi waliowapigia kura kama vile kuanzisha miradi ya maendeleo. Wengine wao huishi mijini bila kwenda kule mashinani kushughulikia mahitaji ya waliowasaidia kufikia vyeo hivyo.

**Kuanguka kwa Viongozi Wasiowajibika**

Katika *Sungura Mpanda Ngazi,* wanyama walisubiri chini wakiwa na matumaini kuwa Sungura atawaonea huruma na kuwaangushia maembe. Subira yao haikuvuta heri. Sungura aliendelea kula maembe peke yake juu ya mwembe huku wanyama waliomsaidia kuukwea mwembe wakiumia kwa njaa. Wanyama walipokata tamaa ya kupata maembe, waliamua kuondoa ngazi waliyokuwa wamemwekea Sungura kwenye mwembe. Kwa hasira, waliiangusha na kuivunjavunja ngazi hiyo. Sungura aliposhuhudia hayo akang'amua kuwa wanyama hawakuwa na mchezo. Ujanja wa Sungura uliisha na akawa anajuta. Hatimaye, siku moja, Sungura aliporomoka kutoka mtini akaanguka na kufa. Sawa na kitendo hiki cha wahusika wanyama, wananchi wakichoshwa na vitendo vibaya vya kiongozi waliyemchagua wanaweza kuamua kwamba hawatamchagua tena. Kiongozi anayewatumia wapiga kura kujinufaisha mwenyewe na kuwapuuza waliomsaidia kufikia mazuri aliyo nayo atakosa kura zao siku za baadaye na kuporomoka.

## Maridhiano na Amani

Juhudi za kutafuta maridhiano na amani zinadhihirika katika *Urembo wa Ngiri.* Mwishoni mwa hadithi, safari ya maridhiano inaanza. Wanyama walikuwa wamepigana, wakaumizana, kuuana na kuchomeana vichaka. Nyani alijtolea kuwauliza wanyama maswali mengi, ikiwa ni pamoja na kutaka kujua kuhusu kilichowapelekea kujiumiza na kupigana. Kobe alijaribu kuwahimiza wenzake waongozwe na falsafa ya kuwa wanyama wote ni sawa. Njiwa alizipiga jeki juhudi za kuleta maridhiano alipopendekeza kuwe na mkutano kati ya Chui na Ngiri, wazo ambalo lilikubaliwa na wanyama wote. Baada ya siku mbili, wanyama wakakutana na kuanza mazungumzo. Kobe akiwa mwenyekiti wao. Mkutano huo ulipendekeza kuwe na Kamati ya Amani ya Wanyama. Chui na Ngiri walishauriwa wakomeshe mapigano mara moja na kuwe na chuo cha kujifunza lugha za wanyama wote wa mwitu. Lugha za Kingiri na Kichui zingekuwa za lazima. Kasuku alichaguliwa kuwa mwalimu mkuu wa lugha. Kila mnyama alihitajika kuelewa lugha ya mwenzake. Matokeo ya mkutano wa Kamati wa Amani yalikuwa kwamba Chui na Ngiri wagawane mamlaka ya ushindi wa urembo. Kila mmoja kati ya Ngiri na Chui angefurahia taji la ushindi kwa muda wa miezi sita. Ngiri alikubali ingawa shingo upande kwa ajili ya kuleta amani nyikani. Chui alipiga magoti na kumwomba Ngiri msamaha kwa kitendo alichowatendea watoto wake. Ngiri pia aliomba msamaha. Hatimaye walisalimiana na kakumbatiana. Walikubali kukomesha uhasama wao. Wanyama wengine walishangilia tukio hilo kwa vifijo na nderemo. Ukurasa mpya ukawa umefunguliwa na kwa mara ya kwanza tangu rabsha izuke wanyama wakaonja utamu wa amani.

## Hitimisho

Makala haya yameonyesha kuwa fasihi ya watoto ina nafasi muhimu katika umoja na mshikamano wa kitaifa nchini Kenya. Fasihi hii inaweza kuwa wenzo wa kumwezesha mtoto kuelewa masuala ya kisiasa yanayomzingira katika jamii. Kusoma hadithi zilizobeba itikadi za kisiasa kutamwezesha mtoto kuwa na ufahamu kuhusu siasa nzuri na kuepuka siasa mbaya. Hadithi zinazoonyesha hasara ya uhasama wa kisiasa na kuhimiza maridhiano na umoja baina ya jamii mbalimbali kama ilivyo katika *Urembo wa Ngiri,* zinaweza kuchangia pakubwa kudumishwa kwa mshikamano wa kitaifa kwa vile watoto wanaozisoma wanaweza kuathiriwa nazo na kuchukua mielekeo ifaayo ya kisiasa na kuweza kuthamini mshikamano wa kitaifa. Hivyo, kama wasemavyo wahenga, samaki mkunje angali mbichi, masuala ya kisiasa yasiachiwe tu fasihi ya watu wazima kwa kuwa ni masuala yanayoathiri maisha ya kila siku ya jamii ambamo mtoto anaishi na kuyashuhudia.

## Marejeleo


Escarpit, R. (1966). *Sociology of Literature*. London: Frank and Cass.

FIDA- K. (2008) *Tume ya Kitaifa ya Upatanishi na Maridhiano*. Nairobi: FIDA.

Grenby, M. O. (2008). *Children's Literature*. Edinburg: Edinburg University Press.

Hunt, P. (mh) (1994) *An Introduction to Children Literature*. New York: Oxford University Press.

Kobia, J. (2008). *Sungura Mpanda Ngazi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kobia, J. (2016). *Urembo wa Ngiri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kriegler na Waki (2009). *Reports on 2007 Elections*. Nairobi.

Matundura, B. (2007). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Miricho, E. M. na Mbuthia, E. M. (2017). "The impact of the depiction of children in selected Swahili children stories" katika *The International Journal of Contemporary Applied Sciences*. Vol 4, No. 1, January, 2017 (ISSN: 2308-1365).

Miricho, E. M. (2015). Usawiri wa watoto katika hadithi za "Mwepesi wa Kusahau" na "Likizo ya Mkosi". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Ngugi, P. M. (2009). *The State of Children Literature in Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Vienna, Austria.

Ngugi, P. M. (2012). "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati." Katika: S. Omari na G. Mrikaria (wh) *Mulika*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Na. 31. 2012 12 - 26 ISBN 0856-0129.

Ngugi, P. M. (2014). "Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia." Katika: D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (wh) *Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Studies* (TATAKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vol. 77. 2014 170-180 ISBN 0856-048 X.

Odaga, A. B. (1985). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchangunuzi wa Fasihi*. Nairobi: Video-muwa Publishers.

Warren, A. na Wellek, R. (1973).*Theory of Literature.* London: Penguin Books.